JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
MTIHANI WA STASHAHADA YA UALIMU WA SEKONDARI

715 **ELIMU YA DINI YA KIISLAMU**

Muda: Saa 3:30 **Year: 2020**

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C zenye jumla ya maswali **kumi na saba (17)**.
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu A, maswali **matatu (3)** kutoka sehemu B na maswali **mawili (2)** kutoka sehemu C.
3. Sehemu A ina alama **40**, sehemu B na C zina alama **30** kila moja.
4. Simu za mkononi na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.



Scanned with CamScanner

SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Eleza kwa ufupi vipengele viwili vinavyoonesha mtazamo potofu juu ya lengo la ibada maalumu.
2. Bainisha hatua mbili zinazotuonesha kushuka kwa Qur'an.
3. Taja vitabu viwili vya hadithi vilivyoandikwa wakati wa maswahaba na viwili vilivyoandikwa wakati wa Tabi'ina.
4. Kwa kutoa mifano, tofautisha kati ya maji mutlak na maji mengi.
5. Andika mambo manne muhimu ya kuzingatia wakati wa kuhakiki kitabu cha kiada.
6. Toa hoja nne zinazomtofautisha mwanadamu na sokwe.
7. Andika faida nne zitakazopatikana endapo mwanadamu atafuata sheria kwa hiari.
8. Orodhesha vitabu vinne mashuhuri vya hadithi na majina ya waandishi wake.
9. Orodhesha malengo manne ya ndoa ya Kiislamu.
10. Taja vitendo vinne vya ufundishaji katika hatua ya utangulizi wa mada mpya.

SEHEMU B (Alama 30)

Jibu maswali **matatu (3)** kutoka sehemu hii.

11. Kwa kutoa mifano iliyomo katika Qur'an, onesha kuwa mpangilio wa Qur'an ni uthibitisho kuwa Qur'an ni kitabu cha Mwenyezi Mungu.
12. Kwa kurejea Qur'an, fafanua hoja tano kuonesha umuhimu wa Elimu katika Uislamu.
13. "Ibada katika Uislamu ina faida nyingi za kijamii, za kinafsi (kiroho) na kiafya kwa mwanadamu, kwani zinafanya mtu aweze kuepukana na kibri na hadaa". Chambua faida zinazopatikana kwa muislamu atakayetekeleza nguzo tano za Kiislamu.
14. Eleza hoja nne alizozitumia Nabii Ibrahim katika kuthibitisha kuwepo kwa Allah (sw) na uwezo wake.

Scanned with CamScanner

SEHEMU C (Alama 30)

Jibu maswali **mawili (2)** kutoka sehemu hii.

15. Fafanua hatua nne katika utengenezaji na utumiaji wa zana za kufundishia na kujifunzia somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu.

16. Fafanua mambo manne kuonesha tofauti kati ya mbinu za kufundishia na kujifunzia kwa njia ya mhadhara na ile ya kutumia jopo la wataalamu.

17. Onesha jinsi utakavyowaongoza wanafunzi kutofautisha kati ya masharti manne ya udhu na nguzo nne za udhu.

Scanned with CamScanner